**UMOJA WA WAKUU WA SHULE TANZANIA (TAHOSSA)**
**HALMASHAURI YA MJI BARIADI**
**MTIHANI WA PAMOJA KIDATO CHA NNE**
**021 KISWAHILI**

---

MUDA: Masaa 2:30 Jumatatu, 28 Machi **2022** mchana
**MAELEKEZO**:

1. *Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D and E.*
2. *Jibu maswali yote.*
3. *Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa bluu au mweusi.*
4. *Vifaa vyote vya mawasiliano visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani.*
5. *Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa sehemu ya juu upande wa kulia.*

## SEHEMU A
## UFAHAMU

***1.Soma kifungu cha habari kifuatacho kisha jibu maswali yafuatayo.***

Miti ina faida nyingi sana kwa binadamu. Nchi isiyo na miti ni sawa na mtu ambaye amevuliwa
nguo. Kuongezeka kwa kasi kwa idadi ya watu na kutokuwepo nishati mbadala hasa sehemu za
vijijini kama vile gesi, umeme nafuu kwa sehemu za mjini kumepelekea kuwepo na matumizi lukuki ya kuni na mkaa katika maisha ya kila siku ya binadamu.

Hali hii imesababisha baadhi ya sehemu ya nchi yetu kuanza kugeuka jangwa kutokana na watu kuzidi kukata miti hovyo kama waswahili wasemavyo “ usipoziba ufa utajenga ukuta” Nchi yetu iliona tatizo hilo na imeanzisha kampeni mbalimbali za kuwahamasisha wananchi kupanda miti kupitia katika vyombo vya habari kama vile redio, magazeti na luninga.

Vilevile imeanza misemo mbalimbali kama vile “ panda mti kata mti” au “ kata mti panda mti” “panda mti wa millennium” na pia imeweka siku maalumu ya kitaifa ya kupanda miti kutokana na kampeni hizo upandaji wa miti nchini umeongezeka kufika miti 120 millioni mwaka huu.

Juhudi za taifa letu katika kampeni hizi zinatokana na ukweli kuwa miti au misitu ni roho ya taifa binadamu hufaidika na mambo mengi yanayotokana na miti. Kutokana na miti watu hujenga nyumba za kila namna wengine hupasua miti mikubwa minene na kupata

mbao na boriti kwa ajili ya kuezekea nyumba, fito zikifungwa na kama nzuri na ngumu, tunapata nyumba imara.

Miti pia hupasuliwa ili kupata mbao za kutengenezea masanduku, kabati, meza na madawati, pia hutumika kutengeneza nyumba ambazo si ghali kama nyumba za matofali ya saruji. Mashua na meli pia hutumia mbao boriti wakati wa kuundwa. Miti huchongwa na kuwa mitumbwi, fimbo, vinu, vinyago, mipini na zana mbalimbali. Kuni zinatumika kwa kupikia, kuchemsha maji na mkaa unatufaa kwa kazi nyingi.

Nchi isiyo na miti haipati mvua, kwani miti hasa misitu husaidia kuvutia mvua. Zaidi ya hayo mizizi ya miti husaidia kushikamanisha udongo hivyo husaidia kuzuia kumomonyoka kwa udongo chemchem za maji pia zinapatikana ikiwa kuna miti ya kutosha na msitu. Magome ya miti na mizizi hutufaa kwa dawa mbalimbali zinazoponya magonjwa mbalimbali. Pengine hutia nguvu miili ama hutukinga kwa maadui kama nyoka.

Miti hutupa matunda ambayo ni matamu na ambayo ni mazuri kwa afya ya miili yetu, machungwa, mapapai, maembe ni baadhi tu ya matunda ambayo tunayatumia kama chakula. Ni jukumu la kila mtu kuhifadhi miti na misitu yetu.

**MASWALI**

(a)(i) Andika kichwa cha habari kisichozidi maneno matano (5).

(ii) Kwa nini suala la kuongezeka kwa watu na ukosefu wa nishati mbadala ni tatizo kwa nchi yetu?

(iii) Eleza maana ya maneno yaliyopigiwa mstari kama yalivyotumika kwenye habari uliyosoma.

- (a) Lukuki
- (b) Roho
- (c) Chemchem
- (d) Kampeni

(iv) Kwa mtazamo wa mwandishi, Taja jambo moja muhimu linaloweza kuzuia kuwepo kwa jangwa nchini.

(v) Taja njia (3) ambazo zinatumika kuwahamisha wananchi kupambana na ongezeko la jangwa nchini.

(vi) Kwa nini mwandishi anasema miti/ misitu ni roho ya Taifa?

(vii) Taja faida mbili (2) za miti kwa afya ya binadamu.

(viii) Mwandishi ana maana gani anaposema “ usipoziba ufa utajenga ukuta”?

(ix) Ni mafanikio yapi yaliyotokana na uhamasishaji wananchi katika suala la upandaji wa miti nchini?

(x) Mwandishi anaona suala la kutunza miti au misitu ni jukumu la nani?

To Get a full post, click *here* and then find a post in our Group as titled in this post!